JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

# TAARIFA YA HALI YA DAWA ZA KULEVYA YA MWAKA 2017

# YALIYOMO


YALIYOMO........................................................................................ i
MAELEZO YA WAZIRI........................................................................ v
DIBAJI............................................................................................ vii
FAHARASA...................................................................................... viii
SURA YA KWANZA........................................................................ 1
1 Utangulizi.................................................................................... 1
1.1 Maboresho na Marekebisho ya Sheria....................................... 1
1.1.1 Sheria kuwa kimya katika masuala ya kihalifu na kutoweka adhabu kwa baadhi ya makosa.................................................. 1
1.1.2 Mamlaka kutokuwa na uwezo wa kumiliki na kutumia silaha. 2
1.1.3 Sheria kutoipa Mamlaka nguvu ya kuchunguza makosa mengine yanayohusiana na dawa za kulevya........................................... 2
1.1.4 Mamlaka kutokuwa na uwezo wa kufanya uchunguzi wa sayansi jinai........................................................................................ 2
1.1.5 Mamlaka kutokuwa na uwezo wa kupata taarifa toka taasisi nyingine...................................................................................... 3
1.1.6 Kamishna Jenerali kutokuwa na uwezo wa kuzuia akaunti za watuhumiwa............................................................................... 3
1.1.7 Dhamana kwa watuhumiwa wa dawa za kulevya...................... 3
1.1.8 Mrundikano wa kesi Mahakama Kuu........................................ 4
1.1.9 Mapungufu yanayotokana na sehemu ya utaifishaji mali......... 4
SURA YA PILI................................................................................. 6
2 TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI.................................. 6
2.1 Utangulizi.................................................................................. 6
2.2 Matumizi na Uzalishaji wa Dawa za Kulevya Duniani............. 6
2.3 Watumiaji wa Dawa za Kulevya................................................. 11
2.4 Ukamataji wa Dawa za Kulevya Duniani.................................. 12
2.5 Uhalifu na Biashara ya Dawa za Kulevya.................................. 13
SURA YA TATU.............................................................................. 17
3 TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA NA UDHIBITI WAKE NCHINI ........................................................................................................ 17
3.1 Utangulizi.................................................................................. 17
3.2 Tatizo la Biashara ya Dawa za Kulevya..................................... 17
3.2.1 Ukamataji wa bangi na watuhumiwa....................................... 17
3.2.2 Ukamataji wa mirungi na watuhumiwa.................................... 18
3.2.3 Ukamataji wa heroin na watuhumiwa...................................... 19
3.2.4 Ukamataji wa cocaine na watuhumiwa..................................... 20
3.2.5 Uteketezaji wa mashamba ya bangi na mirungi........................ 22

3.3 Udhibiti wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya..... 22
3.3.1 Kemikali bashirifu.......................................................................... 22
3.3.2 Udhibiti wa dawa tiba zenye asili ya kulevya.............................. 24
3.4 Tatizo la matumizi ya dawa za kulevya..................................................... 24
3.4.1 Takwimu za Watumiaji................................................................... 24
3.4.2 Madhara ya dawa za kulevya........................................................ 25
3.4.3 Uelimishaji.......................................................................................... 27
3.5 Upunguzaji madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya (Harm reduction)........................................................................................ 29
3.5.1 Tiba ya methadone.......................................................................... 29
3.5.2 Nyumba za upataji nafuu (sober house)....................................... 30
3.6 Masuala Mtambuka........................................................................................ 32
SURA YA NNE.................................................................................................... 34
4 CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA BAADAYE................................ 34
4.1 Changamoto............................................................................................ 34
4.2 Mikakati................................................................................................... 35

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1: Dawa za Kulevya Zilizokamatwa Duniani Mwaka 2015.................... 12

Jedwali 2: Idadi ya Watuhumiwa na Kiasi cha Bangi
Kilichokamatwa 2007 - 2017 ........................................................................ 17

Jedwali 3: Idadi ya Watuhumiwa na Kiasi cha
Mirungi Kilichokamatwa 2007 - 2017.................................................................. 19

Jedwali 4: Idadi ya Watuhumiwa na Kiasi cha
Heroin Kilichokamatwa 2007 - 2017.................................................................... 20

Jedwali 5: Idadi ya Watuhumiwa na Kiasi cha
Cocaine Kilichokamatwa 2007 - 2017.................................................................. 21

Jedwali 6: Waraibu Waliopata Huduma ya
Methadone Tangu Kuanzishwa Hadi Mwaka 2017............................................. 30

Jedwali 7: Waraibu Waliopata Huduma ya
Methadone Nchini Januari - Desemba 2017........................................................ 30

Jedwali 8: Mikoa Yenye Nyumba za Upataji
Nafuu Zinazotambuliwa na Mamlaka.................................................................. 31

# ORODHA YA GRAFU

Grafu 1: Idadi ya Watuhumiwa na Kiasi cha
Bangi Kilichokamatwa 2007 - 2017........................................................................ 18

Grafu 2: Idadi ya Watuhumiwa na Kiasi cha
Mirungi Kilichokamatwa Nchini 2007 - 2017...................................................... 19

Grafu 3: Idadi ya Watuhumiwa na Kiasi cha
Heroin Kilichokamatwa 2007 - 2017..................................................................... 20

Grafu 4: Idadi ya Watuhumiwa na Kiasi cha
Cocaine Kilichokamatwa 2007 - 2017.................................................................... 21

# MAELEZO YA WAZIRI

Tatizo la dawa za kulevya linaathiri nyanja zote zikiwemo afya, jamii, uchumi, siasa pamoja na ulinzi na usalama wa nchi yetu. Kwa kutambua athari zinazosababishwa na tatizo la dawa za kulevya, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ilipendekeza Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na.5 ya Mwaka 2015 ambayo ilipitishwa na Bunge na kuanza kutumika mwezi Septemba 2015.

Pamoja na kutunga sheria na jitihada zingine, nchi yetu iliendelea kukabiliwa na biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Dawa ya kulevya inayotumika zaidi nchini ni bangi ikifuatiwa na heroin, viyeyushi, mirungi na cocaine. Katika siku za hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la matumizi mabaya ya dawa tiba zenye asili ya kulevya. Aidha, serikali ilibaini kuwepo kwa uingizaji, utunzaji na utumiaji holela wa kemikali bashirifu unaoweza kusababisha uchepushaji wa kemikali hizo na kuweza kutengeneza dawa za kulevya.

Kwa kutambua ukubwa wa athari zinazosababishwa na tatizo la dawa za kulevya, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje imefanya jitihada mbalimbali za kukabiliana na tatizo hilo. Jitihada hizo ni pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa taarifa za kiintelijensia; ukamataji wa wauzaji na wasambazaji wakubwa wa dawa za kulevya na kuwachukulia hatua wasiofuata taratibu za uingizaji, utunzaji, usambazaji na utumiaji wa kemikali bashirifu. Aidha, elimu ilitolewa kwa umma juu ya tatizo la dawa za kulevya na kuendeleza utoaji wa tiba kwa waathirika.

Serikali ilikamilisha maboresho na marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya mwaka 2015 kwa Sheria Na. 15 ya mwaka 2017. Maboresho haya yameongeza nguvu katika kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya.

Hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kupambana na dawa za kulevya kupitia wadau wake zimeleta matokeo chanya yakiwemo kukamatwa kwa kiasi kikubwa cha dawa za kulevya, kukamatwa kwa wasambazaji papa wa dawa za kulevya hapa nchini na Duniani kwa ujumla na kuongezeka kwa vituo vinavyotoa huduma kwa waraibu.

Napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza wadau wote kwa kutoa ushirikiano katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya nchini. Kwakuwa tatizo la dawa za kulevya ni mtambuka na linahitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali kuanzia

ngazi ya familia, jamii na Taifa kwa ujumla, ni wajibu wa kila mmoja kwa nafasi yake kuchukua hatua kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya nchini.

Jenista Joakim Mhagama (Mb)
**Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu**
**(Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu)**

# DIBAJI

Kifungu cha 60 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015, kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 15 ya mwaka 2017 kinaielekeza Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuandaa na kuiwasilisha bungeni Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya kila mwaka. Taarifa hii inaonesha hali ya tatizo la dawa za kulevya na jitihada zilizofanyika katika kukabiliana nalo kwa mwaka 2017.

Taarifa hii imegawanyika katika sura kuu nne. Sura ya kwanza inaeleza maboresho na marekebisho ya sheria inayoongeza nguvu katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Sura ya pili inaelezea mwenendo wa tatizo la dawa za kulevya duniani, aina za dawa zinazotumika zaidi zikiwemo dawa zenye asili ya mimea na dawa za viwandani kulingana na upatikanaji wa dawa hizo katika maeneo husika. Sura hii pia inaelezea maambukizi ya magonjwa mbalimbali kwa watumiaji wa dawa za kulevya.

Sura ya tatu imejikita kwenye kuelezea tatizo la dawa za kulevya nchini pamoja na jitihada zilizofanyika kudhibiti biashara haramu ya dawa za kulevya, usambazaji na matumizi ya dawa hizo pamoja na udhibiti wa kemikali bashirifu. Aidha, takwimu za watumiaji wa dawa za kulevya na madhara yatokanayo na dawa za kulevya vimeainishwa. Sura hii pia imeeleza uelimishaji na tiba inayofanyika kwa waathirika wa dawa za kulevya nchini.

Sura ya nne inakamilisha taarifa hii kwa kuainisha changamoto na mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo katika udhibiti na mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya nchini kwa mwaka 2017.

Mwisho napenda kuchukua fursa hii kutoa shukran zangu za dhati kwa wadau wote waliowasilisha taarifa za mapambano dhidi ya dawa za kulevya katika maeneo yao ambazo zilifanikisha uandaaji wa taarifa hii.



Rogers William Siyanga
**KAMISHNA JENERALI**
**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA**
**KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

# FAHARASA

| | |
|---|---|
| CND | The Commission on Narcotic Drugs |
| DCEA | Drug Control and Enforcement Authority |
| GCLA | Government Chemist Laboratory Authority |
| INCB | International Narcotics Control Board |
| LSD | Lysergic Acid Diethylamide |
| MDM | 3,4-methylene-dioxy-methamphetamine |
| MRC | Morogoro Recovery Community |
| NPS | New Psychoactive Substances |
| PEDDEREF | People with Drug Dependence Relief Foundation |
| TFDA | Tanzania Food and Drugs Authority |
| TPA | Tanzania Ports Authority |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| UNAIDS | United Nations Programme on HIV and AIDS |
| UNODC | United Nations Office on Drugs and Crime |
| VVU | Virusi Vya Ukimwi |
| WHO | World Health Organization |

# SURA YA KWANZA

## 1 Utangulizi

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Drug Control and Enforcement Authority) ilianzishwa chini ya Kifungu cha 3 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015. Mamlaka ilianza kazi rasmi mwezi Februari, 2017 baada ya kuteuliwa Kamishna Jenerali ikiwa na majukumu ya kufafanua, kuhamasisha, kuratibu na kutekeleza hatua zote zinazoelekezwa katika udhibiti wa dawa za kulevya.

Katika kutekeleza majukumu yake, Mamlaka imepewa uwezo wa kukamata, kupekua na kupeleleza makosa yanayohusiana na dawa za kulevya kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola ili kuongeza ufanisi wa udhibiti wa dawa za kulevya. Katika kupambana na tatizo hili, Mamlaka inazingatia misingi mikuu mitatu (3) ambayo ni kupunguza uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini (supply reduction); Kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya nchini (demand reduction) na kupunguza madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya (harm reduction).

### 1.1 Maboresho na Marekebisho ya Sheria

Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya 2015 ilitungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Aprili mwaka 2015 na ilianza kutumika tarehe 15 Septemba, 2015. Baada kutumika kwa takribani miaka miwili kulijitokeza changamoto nyingine za kisheria ambazo ama zilisahaulika kufanyiwa kazi au zilijitokeza wakati wa utekelezaji wake hivyo kuathiri juhudi za kupambana na kudhibiti dawa za kulevya nchini ikiwemo udhibiti wa uchwepushaji na uingizaji usio halali wa kemikali bashirifu. Kutokana na changamoto hizi Sheria hii ilifanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya namba 15 ya mwaka 2017 (Drug Control and Enforcement [Amendment] Act No. 15 of 2017) ambayo ilianza kufanya kazi tarehe 01 Desemba, 2017 kwa kutangazwa kwenye gazeti la Serikali Na. 48/2017. Baadhi ya mapungufu na marekebisho yake ni kama ifuatavyo:-

#### 1.1.1 Sheria kuwa kimya katika masuala ya kihalifu na kutoweka adhabu kwa baadhi ya makosa

Katika kushughulikia kesi zinazohusiana na dawa za kulevya ilibainika kuwa kuna mapungufu kwenye Sheria kwa kutoharamisha baadhi ya vitendo vya kihalifu na kutotoa adhabu kwa baadhi ya vifungu vinavyounda makosa. Mfano, kuchepusha au kushughulika isivyo halali na kemikali bashirifu; kuwaweka watu rehani kwa ajili ya biashara ya dawa za kulevya; baadhi ya vifungu

kutotengeneza makosa kutokana na makatazo au wajibu uliowekwa kisheria na baadhi ya vifungu vya Sheria kutengeneza makosa bila kuweka ukomo wa adhabu za chini hivyo kuwepo uwezekano wa kutumika vibaya kwa kutolewa adhabu zisizoendana na ukubwa wa kosa.

Marekebisho ya sheria yametengeneza makosa mapya ili kuziba mianya iliyokuwa wazi bila kushughulikiwa na sheria pamoja na kuweka adhabu kwa baadhi ya makosa yasiyokuwa na adhabu.

### 1.1.2. Mamlaka kutokuwa na uwezo wa kumiliki na kutumia silaha

Wafanyabiashara wa dawa za kulevya humiliki silaha ili kujiwekea kinga ya ulinzi wakati wote hivyo kufanya mazingira ya kiutendaji ya Mamlaka kuwa hatarishi wakati wa utekelezaji wa majukumu yao. Awali Mamlaka ilikuwa ikiomba msaada askari wenye silaha kutoka vyombo vingine vya ulinzi wakati wa kufanya operesheni zake. Utaratibu huu ulilazimu operesheni za Mamlaka kujulikana kwa watendaji wengi hivyo kusababisha uvujishaji wa siri kwa watendaji wasio waadilifu na kuathiri operesheni. Aidha, baadhi ya taarifa zilipatikana nyakati za usiku na kuhitaji utekelezaji wa haraka, maafisa wa Mamlaka ama walijitoa muhanga na kuhatarisha maisha yao au kughairisha ukamataji na hivyo kutoa mwanya kwa wafanyabiashara wa dawa za kulevya kuendelea kufanya biashara hizo kwa uhuru. Marekebisho yaliyofanyika ni kuipa uwezo Mamlaka kumiliki na kutumia silaha.

### 1.1.3. Sheria kutoipa Mamlaka nguvu ya kuchunguza makosa mengine yanayohusiana na dawa za kulevya

Kifungu cha 4 cha Sheria kinaelezea Mamlaka au mambo ambayo Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ingeweza kuyashughulikia. Hata hivyo kifungu kidogo cha (2) aya (f) hakikuweka bayana uwezo wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kushughulikia makosa mengine inayokutana nayo wakati wa upelelezi wa kesi zake kama vile kughushi na utakatishaji wa fedha haramu. Marekebisho ya sheria yameipa Mamlaka nguvu ya kupeleleza/kushugulikia makosa mengine yanayojitokeza wakati wa ushughulikiaji/uchunguzi wa makosa yotokanayo na dawa za kulevya.

### 1.1.4. Mamlaka kutokuwa na uwezo wa kufanya uchunguzi wa sayansi jinai

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imepewa uwezo wa kuzuia, kubaini na kuchunguza matumizi mabaya ya dawa za binadamu na kemikali ambazo zimeorodheshwa katika dawa zinazodhibitiwa. Ili iweze kufanya hayo Mamlaka ilihitaji kuwa wa wataalamu na maabara yenye uwezo na nguvu ya kisheria ya kuchunguza sampuli za dawa na kemikali hizo ili kurahisisha na kuharakisha upelelezi wa kesi. Upungufu kisheria ulikwamisha

jitihada hizi. Marekebisho ya sheria yaliyofanyika yameipa Mamlaka uwezo wa kufanya uchunguzi wa sayansi jinai.

**1.1.5. Mamlaka kutokuwa na uwezo wa kupata taarifa toka taasisi nyingine**

Mamlaka katika kutekeleza majukumu yake ya kudhibiti dawa za kulevya, kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya ilihitaji kuwa na mfumo wa kupata au kubadilishana taarifa au kufanya mashauriano na taasisi nyingine zinazohusiana na utoaji wa vibali vya kuingiza nchini dawa na kemikali hizo. Kukosekana kwa kifungu cha Sheria kinachowezesha mashauriano kulisababisha kuwepo kwa matumizi mabaya ya dawa au kemikali ikiwemo uchepushaji wa kemikali bashirifu kwa ajili ya utengenezaji wa dawa za kulevya. Marekebisho ya sheria yaliyofanyika yaliipa Mamlaka uwezo wa kupata taarifa toka taasisi nyingine ili kufanikisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

**1.1.6. Kamishna Jenerali kutokuwa na uwezo wa kuzuia akaunti za watuhumiwa**

Sheria haikumpa uwezo Kamishna Jenerali wa kuweka zuio au kushikilia akaunti za benki za watuhumiwa wa dawa za kulevya suala ambalo liliathiri utendaji kazi wa Mamlaka kwa kuongeza mwanya wa watuhumiwa kutorosha au kuhamisha fedha kwa haraka wakati wa uchunguzi. Katika kuchunguza mashauri ya mali na mazalia ya uhalifu Kamishna Jenerali alimtegemea Inspekta Jenerali wa Polisi au Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai kuweka zuio hilo. Baada ya marekebisho ya sheria. Kamishna Jenerali amepewa mamlaka ya kuzuia au kufungia akaunti ya mtuhumiwa kwa muda maalum.

**1.1.7. Dhamana kwa watuhumiwa wa dawa za kulevya**

Kabla ya marekebisho Sheria iliruhusu kutolewa dhamana kwa watuhumiwa wa dawa za kulevya zenye uzito wa chini ya gramu 200 kwa dawa za kulevya za viwandani ambazo ni heroin na cocaine na chini ya kilo 100 kwa bangi na mirungi. Kiwango hicho ni kikubwa ikilinganishwa na madhara yanayoweza kusababishwa na wingi wa dawa hizo. Matokeo yake wafanyabiashara wa dawa hizo walibuni mbinu ya kugawa dawa katika mafungu madogo madogo yasiyozidi gramu 200 wakijua kuwa endapo watakamatwa basi watapata dhamana kwa urahisi kutokana na kigezo cha uzito, hivyo kuweza kuendelea na biashara zao na kuvuruga ushahidi wa kesi zao.

Aidha, kuna baadhi ya makosa makubwa ambayo hayakujumuishwa kwenye makatazo ya kutopata dhamana. Sheria kabla ya marekebisho ilitoa dhamana kwa makosa makubwa ya kumiliki mitambo kwa lengo la kutengeneza dawa za kulevya, kufadhili biashara ya dawa za kulevya na kuwaingiza watoto kwenye biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Makosa haya ni makubwa zaidi

pengine hata kuzidi ya kusafirisha dawa za kulevya.

Marekebisho ya sheria yalihuisha vigezo vya utoaji wa dhamana kwa makosa ya dawa za kulevya ili kuendana na hali halisi inayolenga kukomesha biashara ya dawa za kulevya nchini. Mfano, watuhumiwa wanaowahusisha watoto katika biashara na matumizi ya dawa za kulevya; kuwaweka rehani watanzania kwa minajili ya biashara ya dawa za kulevya; wanaofadhili biashara ya dawa za kulevya na kumiliki mitambo hawatapata dhamana. Aidha, watuhumiwa wote watakaokutwa na kiwango cha zaidi ya gramu 20 kwa cocaine na heroin, kilo 20 kwa bangi na mirungi na kilo 30 au lita 30 za kemikali bashirifu yabisi na kimiminika hawatapata dhamana.

### 1.1.8. Mrundikano wa kesi Mahakama Kuu

Baada ya marekebisho ya Sheria Na. 3 ya Mwaka 2016 yaliyorekebisha Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200, kesi zote za dawa za kuleva zikiwemo zenye uzito mdogo zilifanywa kuwa makosa ya uhujumu uchumi na hivyo kusikilizwa Mahakama Kuu na kusababisha mrundikano Mahakama kuu. Hivyo, kulikuwa kuna haja ya kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ili kuondoa tatizo hilo.

Marekebisho ya Sheria yaliruhusu Mahakama za chini kusikiliza mashauri ya dawa za kulevya zenye uzito mdogo kwa kuanzisha kifungu kipya kilichoainisha makosa yanayohusisha dawa zenye uzito mdogo.

### 1.1.9. Mapungufu yanayotokana na sehemu ya utaifishaji mali

Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya mwaka 2015 iliweka utaratibu wa kufuatwa katika utaifishaji mali na kuitambua Sheria ya Utaifishaji Mali (The Proceeds of Crime Act), sura ya 256. Hata hivyo katika utekelezaji wa sehemu hii yalibainika mapungufu mengi kama ifuatavyo:

a) Kabla ya marekebisho sheria iliongelea utaifishaji wa mali zilizopatikana au kutumika katika biashara ya usafirishaji wa dawa za kulevya lakini iliacha nje mali nyingine mfano za mtu aliyezipata kihalali lakini akazitumia kufadhili biashara ya dawa za kulevya.

b) Kabla ya marekebisho sheria iliangalia mali za watuhumiwa tu na kuacha mali za washirika wake katika biashara ya dawa za kulevya.

c) Kifungu cha 49 (4) kilisema mali haitataifishwa endapo ilipatikana si zaidi ya miaka 5 tangu tarehe ya kushtakiwa kwa makosa ya usafirishaji haramu wa dawa za kulevya. Ukweli ni kwamba muda huo ni mfupi sana.

Marekebisho ya sheria yameruhusu kuweka mfumo mzuri wa ushughulikiaji na taratibu za utaifishaji wa mali na mazalia ya uhalifu, ikiwemo utaifishaji kwa njia ya Kiutawala (Administrative Forfeiture) na Kimahakama (Judicial Forfeiture). Pia muda wa mali inayoweza kutaifishwa umeongezwa kutoka miaka mitano mpaka kumi pamoja na kuhusisha mali za washirika katika biashara ya dawa za kulevya

# SURA YA PILI

## 2 TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI

### 2.1 Utangulizi

Kulingana na Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2017 inakadiriwa kuwa mwaka 2015 takriban watu wazima wapatao milioni 250 ambao ni sawa na asilimia tano ya watu wote duniani walitumia dawa za kulevya na kati yao watu milioni 29.5 walipata matibabu kutokana na matatizo yanayoambatana na matumizi ya dawa hizo. Aidha, vifo vinavyozuilika vipatavyo 190,000 vinakadiriwa kutokea duniani kutokana na matumizi ya dawa za kulevya hasa za jamii ya afyuni. Dawa za kulevya pia zimekuwa zikiathiri afya kwa kuongeza maambukizi ya VVU, homa ya ini na kifua kikuu. Matibabu stahili kwa watumiaji wa dawa za kulevya ni changamoto kwani takwimu zinaonesha ni mraibu mmoja tu kati ya sita anayeweza kupatiwa matibabu kwa mwaka. Hali hii inatokana na ufinyu wa huduma za matibabu kwa waraibu.

Kwa upande wa matumizi ya dawa za kulevya duniani, bangi iliongoza kwa matumizi, ikifuatiwa na dawa za jamii ya afyuni “opioids” kama vile heroin na fentanyl; dawa za jamii ya amfetamini; ecstasy na cocaine. Aidha, dawa za kutengenezwa kwenye maabara haramu zilitawala zaidi soko la nchi zilizoendelea na Bara la Asia kuliko nchi za Afrika.

Sura hii inaainisha matumizi na uzalishaji wa dawa za kulevya zilizotawala soko la dunia, makundi ya watumiaji wa dawa za kulevya na maambukizi ya magonjwa, ukamataji wa dawa za kulevya pamoja na uhalifu unaoambatana na biashara ya dawa za kulevya.

### 2.2 Matumizi na Uzalishaji wa Dawa za Kulevya Duniani

#### 1. Bangi

Bangi imeendelea kuwa dawa ya kulevya inayotumika zaidi ambapo mwaka 2014 ilikadiriwa kutumiwa na takriban watu milioni 183 duniani. Baadhi ya nchi zimeruhusu matumizi ya bangi kwa ajili ya matibabu tu na wengine kwa ajili ya matibabu na starehe. Kwa mfano, mwaka 2013 Serikali ya Uruguay ilikuwa nchi ya kwanza duniani katika zama hizi iliyopitisha sheria iliyoruhusu kilimo, utengenezaji, usambazaji na uvutaji bangi. Taratibu na kanuni mbalimbali ziliwekwa kusimamia matumizi ya bangi kama tiba, soko la bangi na usambazaji wa bangi ya kuvuta kwenye vituo vya uuzaji pamoja na kuwasajili wavutaji.

Vilevile, nchi ya Marekani iliruhusu majimbo yake nane kutoa leseni ya kulima na kuuza bangi kwa matumizi ya matibabu na starehe kati ya mwaka 2012 hadi 2016. Kumekuwa na ongezeko la ujumla la matumizi ya bangi nchini Marekani, lakini maeneo ambayo uvutaji bangi umehalalishwa matumizi yameongezeka kwa watu wazima wenye kipato cha chini ikilinganishwa na maeneo ambako haijaruhusiwa.

Aidha, kumeibuka dawa za kulevya mbalimbali zilizotengenezwa kwenye viwanda au maabara haramu kwa kuiga baadhi ya kemikali zinazopatikana kwenye mmea wa bangi zikijulikana kama "cannabinoids". Dawa hizi ambazo nyingi zina nguvu zaidi ya bangi ya mimea zinapatikana kwa majina mengi zikiwa na aina na viwango tofauti vya kemikali zimekuwa zikileta taharuki katika jamii kutokana na madhara ambayo watumiaji huyapata ikiwemo vifo. Dawa hizi ziinaelezewa zaidi kwenye kipengele cha kundi la Dawa Mpya za Kulevya.

**2. Dawa za kulevya jamii ya afyuni (opioids)**

Kundi hili la dawa za kulevya lilifuatia kwa matumizi duniani katika mwaka 2014 likikadiriwa kuwa na watumiaji milioni 53. Dawa za jamii ya afyuni huhusisha dawa za asili za heroin, morphine, codeine na thebaine zitokanazo na utomvu wa afyuni; oxymorphone, hydrocodone, oxycodone na hydromorphone zitokanazo na uchakataji wa codeine na morphine pamoja na kundi la tatu la dawa zinazotengenezwa za methadone, tramadol, fentanyl na meperidine.

Matumizi ya dawa za kulevya za jamii ya afyuni yanaongoza kwa kusababisha maradhi na vifo ambavyo vinazuilika. Asilimia 70 ya maradhi mbalimbali yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya yalitokana na matumizi ya dawa za kulevya za jamii ya afyuni. Robo ya vifo vyote vitokanavyo na matumizi ya dawa za kulevya duniani hutokea nchini Marekani kutokana na matumizi ya dawa za kulevya jamii ya afyuni. Vifo vinavyotokana na kuzidisha dozi vimeongezeka mara tatu zaidi katika kipindi cha mwaka 1999 hadi 2015 kutoka vifo 16,849 hadi 52,404 kwa mwaka. Vifo hivyo viliongezeka kwa asilimia 11.4 mwaka 2016 kikiwa ni kiwango ambacho hakijawahi kufikiwa na vilizidi vile vinavyotokana na ajali za barabarani na vurugu nyingine nchini humo.

Ikilinganishwa na mwaka 2015, mwaka 2016 kulikuwa na ongezeko la theluthi moja zaidi ya afyuni iliyozalishwa duniani. Ongezeko hili lilitokana na matumizi ya mbinu za kisasa katika kilimo cha mimea ya afyuni nchini Afghanstan iliyozalisha tani 6,380 bila kuongeza ukubwa wa mashamba. Mwaka 2015 kulikuwa na ongezeko la heroin iliyokamatwa katika nchi za Amerika ya

Kaskazini. Ongezeko hili liliambatana na matumizi makubwa ya heroin na vifo vilivyotokana na matumizi yake.

### 3. Metamfetamini

Baada ya dawa za kulevya jamii ya afyuni, dawa za kulevya zinazofuata kwa kusababisha madhara kwa watumiaji ni zile za jamii ya amfetamini zikiwa na wastani wa watumiaji milioni 37 duniani. Katika dawa za jamii ya amfetamini, metamfetamini iliongoza kwa matumizi kutokana na ongezeko la watumiaji wanaotafuta matibabu ya uraibu wa dawa hiyo. Kiasi kikubwa cha metamfetamini huzalishwa kwenye maabara na viwanda haramu vilivyo katika nchi za Mashariki mwa Bara la Asia.

Ukamataji wa dawa za kulevya za jamii ya amfetamini uliongezeka mara mbili katika kipindi cha miaka mitano (5) kabla ya mwaka 2015 na mwaka huo kiasi kilichokamatwa kilifikia tani 191. Katika dawa za jamii ya amfetamini, metamfetamini ndiyo dawa iliyokamatwa kwa wingi zaidi ikifikia asilimia 61 hadi 80 ya ukamataji wote uliofanywa kwa mwaka katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015. Nchi za Asia ya Kusini na Kusini Mashariki pamoja na Oceania zilionesha ongezeko la matumizi ya metamfetamini likidhihirishwa na ongezeko la watumiaji waliokuwa wanapatiwa matibabu ya uraibu wa dawa hiyo. Tofauti na metamfetamini, amfetamini inapatikana katika maeneo machache zaidi hususani Mashariki ya Kati, Ulaya ya Magharibi na Ulaya ya Kati.

### 4. MDMA (3,4-methylenedioxy-methamphetamine)

Dawa hii inafahamika zaidi kama "ecstasy", "molly", "mandy", "superman" ikiwa katika kundi la dawa za kulevya za jamii ya amfetamini zinazotengenezwa katika umbo la vidonge kwenye viwanda au maabara haramu. Mara nyingi dawa hii huchanganywa na dawa nyingine za kulevya na kuhatarisha zaidi afya ya watumiaji au kusababisha vifo. Inakadiriwa kuna watumiaji wapatao milioni 22 duniani waliotumia dawa hii katika mwaka 2014 kiasi ambacho kinazidi watumiaji wa cocaine ambao walikuwa milioni 17 kwa mwaka huo. Kumekuwa na uingizwaji wa aina mbalimbali za dawa hizi kwenye soko la dawa za kulevya ambapo zimegawanyika katika makundi matatu. Kuna Ecstasy zisizo au zenye kiwango kidogo cha MDMA, nyingine zenye kiwango kikubwa cha MDMA na ecstasy zinazouzwa kwa majina mbalimbali. Nchi za Ulaya zimekumbwa na tatizo la ecstasy zenye viwango vikubwa vya MDMA ambapo vyombo vya dola vimeweza kugundua uzalishaji mkubwa wa MDMA.

### 5. Cocaine

Cocaine ambayo hutokana na mmea wa coca unaolimwa katika mabara ya Amerika imeendelea kutumika katika sehemu nyingi duniani ambapo katika

mwaka 2014 ilikadiriwa kuwa na watumiaji milioni 17. Matumizi ya cocaine yameongezeka katika nchi za Amerika ya Kaskazini hususani nchini Marekani. Vifo vinavyotokana na kuzidisha dozi ya cocaine viliongezeka nchini humo katika kipindi cha mwaka 2012 hadi 2015. Ongezeko la vifo hivyo vilitokana na matumizi ya mchanganyiko wa cocaine na dawa za kutengenezwa za jamii ya afyuni.

Katika kipindi cha mwaka 2013-2015 kilimo cha mimea ya coca kiliongezeka kwa asilimia 30 hasa katika nchi ya Colombia. Kiasi cha tani 1,125 cha cocaine kilizalishwa mwaka 2015 kikiwa ni ongezeko la asilimia 25 ya kiasi kilichozalishwa mwaka 2013. Hali hiyo ilienda sambamba na ongezeko la soko la dawa hiyo katika nchi za Ulaya na Amerika ya Kaskazini. Utafiti uliofanyika katika nchi za Ulaya ulibaini ongezeko la matumizi ya cocaine kwa asilimia 30 katika kipindi cha mwaka 2011 hadi 2016. Kiasi cha cocaine kilichokamatwa duniani pia kiliongezeka kwa asilimia 30 na kufikia tani 864 mwaka 2015 pekee, kiwango ambacho hakijawahi kufikiwa. Amerika ya Kaskazini ilikamata tani 141 za cocaine ikiwa ni ongezeko la asilimia 40 na Ulaya ilikamata jumla ya tani 84 ikiwa ni ongezeko la asilimia 35.

Soko la cocaine liliendela kuongezeka kwa kiasi kidogo katika nchi za bara Asia. Hali hii inathibitika kwa ukamataji mkubwa uliofanyika kwenye nchi za Sri Lanka ambapo kilo 900 zilikamatwa mwaka 2016 na kilo 500 zikikamatwa nchini Djibout katika mwaka 2017 zikidhaniwa kusafirishwa kwenda barani Asia. Ukamataji wa kilo 500 nchini Djibout ulikuwa ni ukamataji mkubwa zaidi uliowahi kufanyika kwa mara moja katika eneo la Mashariki ya Afrika tangu mwaka 2014. Mwaka 2015 kulikuwa na ongezeko la asilimia 40 ya ukamataji cocaine katika nchi za Bara la Asia ikilinganishwa na mwaka 2014. Maeneo yaliyoongoza kwa ukamataji wa cocaine Barani Asia ni Asia ya Mashariki iliyokuwa na asilimia 56 na Mashariki ya Kati asilimia 40.

### 6. Dawa mpya za kulevya-NPS

Dawa mpya za kulevya hazidhibitiwi na Mikataba ya Kimataifa ya mwaka 1961 na 1971 kama ilivyo kwa dawa nyingine za kulevya. Watengenezaji huiga kemikali zilizo kwenye dawa za kulevya zinazodhibitiwa kimataifa kama bangi, cocaine, heroin, LSD, MDMA (ecstasy) na metamfetamini. Dawa hizi hutambulika kama vilevi halali yaani "legal highs", dawa zinazotumika kuogea "bath salts" na kemikali za utafiti "research chemicals" ili kuficha ukweli na kukwepa mkono wa sheria.

Nyingi ya dawa hizi si mpya bali zimeingia sokoni hivi karibuni. Sehemu kubwa ya dawa hizi ziliwahi kutumika kwenye tiba hapo awali zikapigwa marufuku au

kutumika kwenye tafiti mbalimbali. Baadaye ziliingizwa kwenye soko la watumiaji waliotaka kujistarehesha pasipo kufuata sheria. Watengenezaji huchanganya kemikali mbalimbali kulingana na matakwa yao bila kujali madhara yanayoweza kumpata mtumiaji na kuzifanya kuwa dawa hatari zaidi kwa watumiaji hao. Pamoja na hatari hiyo hakuna tafiti za kisayansi za kutosha zinazoelezea madhara ya kemikali hizi kwa watumiaji na jamii kwa ujumla hivyo kufanya udhibiti kuwa mgumu. Baadhi ya dawa hizo ni bangi ya kutengenezwa "synthetic cannabinoids", dawa zinazofanana na cathinone inayopatikana kwenye mirungi "synthetic cathinones", dawa za jamii ya aminoindanes, pamoja na dawa zinazotokana na mimea kama mirungi (Catha edulis) na kratom (mitragyna speciosa Korth)

Soko la dawa mpya za kulevya linabadilika kila wakati kutokanana uwepo wa dawa nyingi mpya zinazotengenezwa kila uchao zikitengenezwa kwa kutumia kemikali ambazo hubadilishwa mara kwa mara. Kati ya mwaka 2009 na 2016 nchi 106 duniani zilitoa taarifa ya kuibuka kwa dawa mpya za kulevya zipatazo 739 kwa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC). Dawa hizi huibuka ghafla kwenye soko na baada ya muda mfupi hupotea katika kukwepa udhibiti wake. Dawa hizi hupatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu zaidi ya dawa za kulevya zilizozoeleka. Takwimu zinaonesha kumekuwa na ongezeko la dawa mpya sokoni kutoka dawa 260 mwaka 2012 hadi 483 mwaka 2015.

Aidha, katika kipindi cha mwaka 2009 hadi 2015 kumekuwa na wastani wa dawa mpya zipatazo 80 kila mwaka katika soko la kimataifa hatua iliyosababisha baadhi ya dawa hizo kuanza kudhibitiwa kimataifa. Pia, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2013 dawa nyingine mpya za kulevya zipatazo 60 zilitoweka kwenye soko. Kutoweka huku kunaweza kutokana na kutoweza kugundulika katika maabara na kuwa hazifahamiki kwa wengi hivyo hazitolewi taarifa za uwepo wake.

Dawa za kutengenezwa hazihitaji kuwa na maeneo maalum ya kuzalishia kama ilivyo kwa dawa zinazotokana na mimea ya coca na afyuni ambazo hulimwa. Hivyo hakuna takwimu halisi zinazoonesha kiasi cha dawa hizi kilichozalishwa duniani. Hatahivyo, takwimu za ukamataji zinaonesha ongezeko la uzalishaji wa dawa mpya za kulevya za kutengenezwa ambapo kiasi cha tani 57 kilikamatwa katika mwaka 2015.

## 2.3 Watumiaji wa Dawa za Kulevya

**1. Maambukizi ya Homa ya ini na VVU**

Katika makundi ya watumiaji wa dawa za kuleya, wajidunga ndio wanaoongoza kwa kuathirika zaidi kiafya. Kwani kati ya wajidunga milioni 12 wanaokadiriwa kuwepo duniani zaidi ya nusu ambao ni takribani wajidunga milioni 6.1 wanaishi na virusi vya homa ya ini aina C, moja ya nane kati yao ambao ni watu milioni 1.6 wanaishi na maambukizi ya VVU na wengine milioni 1.3 wakiwa na maambukizi yote mawili ya VVU na homa ya ini aina C. Vilevile, vifo kwa watumiaji wa dawa za kulevya wenye maambukizi ya homa ya ini aina C ni vingi zaidi ambapo vimekadiriwa kufikia 222,000 ikilinganishwa na 60,000 kwa wenye maambukizi ya VVU. Ingawa hivi karibuni kumekuwa na dawa za kupunguza makali ya virusi vya homa ya ini aina C bado tiba hiyo haiwanufaishi wengi kwa kuwa ni ghali.

**2. Maambukizi ya ugonjwa wa kifua kikuu**

Ugonjwa wa kifua kikuu ni moja ya maradhi yanayowapata zaidi watumiaji wa dawa za kulevya kuliko watu wengine. Katika tafiti zilizofanyika katika nchi za Ulaya, Asia na Amerika ilikadiriwa asilimia nane (8) ya wajidunga wa dawa za kulevya walikutwa na ugonjwa huo ikilinganishwa na wastani wa asilimia 0.2 ya maambukizi katika jamii. Ni rahisi zaidi kwa wajidunga wanaoishi na VVU kuambukizwa ugonjwa wa kifua kikuu.  Ugonjwa wa kifua kikuu unaongoza kwa kusababisha vifo kwa wajidunga wanaoishi na VVU. Sababu nyingine zinazochangia ongezeko la ugonjwa wa kifua kikuu kwa watumiaji wa dawa za kuleya ni kuwa na afya dhoofu, umasikini na utumikiaji wa vifungo jela. Watumiaji wa dawa za kulevya wenye ugonjwa wa kifua kikuu ni vigumu kunufaika na tiba yake ambayo huchukua muda mrefu na ina masharti mengi ikizingatiwa kuwa pamoja na kuwa na ugonjwa huo wanaweza kuwa na maambukizi ya VVU, homa ya ini, magonjwa ya afya ya akili pamoja na uraibu wa dawa za kulevya.

**3. Matumizi ya dawa za kulevya kwa wafungwa**

Dawa za kulevya pia hutumika kwenye magereza. Tafiti zinaonesha wastani wa mfungwa mmoja kati ya watatu waliwahi kutumia dawa za kulevya. Bangi inaongoza kwa matumizi ikifuatiwa na heroin. Asilimia kumi (10) ya wafungwa waliwahi kutumia heroin wakiwa kifungoni. Wajidunga wanapofungwa huongeza hatari ya magonjwa ambukizi kwa njia ya damu kutokana na uhaba wa sindano safi katika mazingira ya jela na kuongeza maambukizi ya VVU miongoni mwao na jamii inayowazunguka.

**4. Matumizi ya dawa za kulevya kwa wanawake**

Ingawa idadi ya wanaume wanaotumia dawa za kulevya ni mara mbili au zaidi ya wanawake, wanawake huathirika zaidi na kuwa wategemezi au waraibu kwa haraka zaidi ya wanaume. Hii ni kwa sababu wanawake wanapoanza matumizi ya dawa za kulevya au pombe huongeza kiwango wanachotumia kwa haraka zaidi ya wanaume. Halikadhalika, ni rahisi kwa wanaume kupata huduma za matibabu kuliko wanawake watumiaji. Hivyo wanawake wanaotumia dawa za kulevya huathirika zaidi kiafya kuliko ilivyo kwa wanaume watumiaji.

## 2.4 Ukamataji wa Dawa za Kulevya Duniani

Ushirikiano wa vyombo vya dola kimataifa umeonesha mafanikio kwani kumekuwa na ongezeko la dawa za kulevya zinazokamatwa kimataifa. Mfano, katika mwaka 2015 ukamataji wa cocaine kimataifa ulivunja rekodi ambapo uliongezeka kwa kati ya asilimia 45 na 55 ya ukamataji wa miaka ya nyuma. Ukamataji wa dawa za kulevya za jamii ya afyuni nao uliongezeka kwa asilimia kati ya 23 na 32 katika kipindi cha mwaka 2009 hadi mwaka 2015.

Kiasi cha heroin na morphine kilichokamatwa katika nchi za Bulgaria, Ugiriki and Uturuki katika kipindi cha miaka ya 2014-2015 kilipungua ikilinganishwa na kiasi kilichokuwa kinakamatwa katika miaka ya 2012-2013. Hali hii inawezekana kuwa ilisababishwa na wasafirishaji kubadilisha njia kutokana na wingi wa wakimbizi wanaokimbilia nchi za Ulaya. Hali ilikuwa tofauti kwa njia inayounganisha nchi za Armenia, Azerbaijan, Georgia, Ukraine na Romania ambapo kiasi cha heroin na morphine kilichokamatwa kiliongezeka katika vipindi hivyo viwili. Ukamataji wa dawa mbalimbali za kulevya katika mwaka 2015 umeainishwa kwenye jedwali lifuatalo:-

Jedwali 1: Dawa za Kulevya zilizokamatwa Duniani Mwaka 2015

| Na. | Dawa ya kulevya | Kiasi (Tani) |
|---|---|---|
| 1. | Bangi (majani na hashish) | 7 317 |
| 2. | Cocaine | 864 |
| 3. | Afyuni ya utomvu- Opium | 587 |
| 4. | Metamfetamini | 132 |
| 5. | Dawa tiba jamii ya afyuni (pharmaceutical opioids) | 113 |
| 6. | Heroin na morphine | 90 |
| 7. | Dawa mpya za kulevya za viwandani (NPS) | 57 |
| 8. | Amfetamini | 52 |
| 9. | Ecstasy | 6 |

Usafirishaji wa dawa za kulevya umehamia katika njia ya Balkan inayopitia katika nchi za Caucasus (Armenia, Azerbaijan, Georgia, Iran na Russia) zikiikwepa Uturuki. Uturuki imekumbwa na wimbi la wakimbizi wanaokimbilia nchi za Ulaya na kuwafanya wafanyabiashara wa dawa za kulevya kubadilisha njia. Hatahivyo, njia ya Balkan imeendelea kuwa kitovu cha usafirishaji wa afyuni ambapo asilimia 40 ya ukamataji wote uliofanyika duniani katika mwaka 2015 ulikuwa katika nchi inakopita njia hiyo. Kiasi cha heroin na morphine kilichokamatwa kwenye njia ya zamani ya Balkan inayopitia katika nchi za Bulgaria, Ugiriki na Uturuki kilipungua katika kipindi cha miaka ya 2014 hadi 2015 ikilinganishwa na kiasi kilichokamatwa kwenye miaka ya 2012 hadi 2013. Hatahivyo, kiasi cha heroin na morphine kilichokamatwa kwenye njia mpya ya Balkan inayopitia katika nchi za Ulaya za Armenia, Azerbaijan, Georgia, Ukraine na Romania kiliongezeka katika vipindi hivyo.

### 2.5 Uhalifu na Biashara ya Dawa za Kulevya

Pamoja na makundi ya kihalifu kujihusisha na biashara ya kimataifa ya dawa za kulevya, mengi kati yao yameongeza wigo wa uhalifu kwa kujihusisha na uhalifu mwingine ikiwemo uhalifu wa kimtandao, biashara ya nyara za serikali, uvuvi haramu, ukataji wa miti, uchafuzi mkubwa wa mazingira, biashara ya kemikali zinazoharibu utando wa "ozone", n.k. Utafiti uliofanywa na "Ueropol" kwa wauza dawa za kulevya kwenye nchi za Umoja wa Ulaya unaonesha karibu theluthi moja wanajihusisha na uhalifu mwingine ikiwemo biashara ya bidhaa (feki/bandia/zilizo chini ya viwango), biashara ya binadamu, silaha na usafirishaji wahamiaji kimagendo.

Katika magenge 5,000 ya kihalifu ya kimataifa yaliyogunduliwa na "Europol" kwenye nchi za Umoja wa Ulaya mwaka 2017, theluthi moja yalikisiwa kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya. Hii inaashiria kuwa biashara ya dawa za kulevya ni shughuli iliyoenea zaidi kwa wahalifu wa kimataifa kuliko ilivyo kwa usafirishaji wa binadamu, utapeli, usafirishaji kimagendo wa wahamiaji, nk.

Magenge makubwa ya kihalifu yenye ngazi za uongozi madhubuti ya nchi za Mexico, Japan na Russia yameendelea kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya hasa katika nchi za Ulaya. Hatahivyo, kumeibuka vikundi vidogo vya uhalifu wa kimataifa ambapo mwaka 2017 "Europol" ilikadiria asilimia kati ya 30 hadi 40 ya uhalifu wote uliofanyika katika nchi za Umoja wa Ulaya ulifanywa na vikundi hivyo.

**1. Mitandao ya siri ya biashara ya dawa za kulevya**

Maendeleo katika sekta ya mawasiliano yameleta neema kwa wauza dawa za kulevya kwani dawa za kulevya huweza kuuzwa na kununuliwa wakitumia mtandao wa siri bila ya wahusika kufahamiana wala kubainika kwa vyombo vya dola. Aidha, badala ya wanunuzi wa dawa za kulevya kutumia fedha za kawaida huweza kutumia fedha za kidigitali "bitcoins"ambazo hazipitii benki na hazina msimamizi anayeziratibu. Dawa za kulevya zilizozoeleka kununuliwa kwa mitandao hii ni bangi, ecstasy, cocaine, hallucinogens na dawa mpya za kulevya. Ingawa mauzo ya dawa za kulevya kwa njia hii ni madogo lakini yanaongezeka katika nchi zilizoendelea.

**2. Utakatishaji wa fedha**

Asilimia 30 ya mauzo ya cocaine iliingia katika mtiririko wa fedha haramu. Aidha, UNODC iligundua kuwa asilimia 30 ya mauzo ya cocaine duniani yalitakatishwa na kupelekwa nje ya nchi husika katika mwaka 2009. Vilevile, utafiti ulifanyika mwaka 2016 kwa wahalifu wa dawa za kulevya waliokuwa magerezani nchini Italia uligundua kuwa theluthi moja ya fedha iliyokuwa inatumiwa kununulia cocaine ilitokana na fedha iliyotakatishwa nje ya nchi hiyo.

Biashara ya dawa za kulevya hudhoofisha uchumi wa nchi husika. Ukiangalia kwa haraka utafikiri kuwa fedha itokanayo na biashara ya dawa za kulevya itaongeza pato la ndani la nchi, la hasha. Fedha zitokanazo na biashara ya dawa za kulevya zinapochukua asilimia kubwa ya uchumi huongeza bei ya mali zisizohamishika, huvuruga biashara ya nje, huondoa ushindani kwenye biashara, huongeza tofauti ya vipato na kuongeza rushwa. Kwa hiyo wale wanaofanyakazi halali watashindwa kufanya biashara na kuondoka kwenye soko kwa kushindwa kushindana na wafanyabiashara ya dawa za kulevya. Matokeo yake utawala wa sheria hautakukwepo, rushwa itatawala na hatimaye fedha inayopatikana itatumika kuimarisha biashara ya dawa za kulevya. Tafiti zinaonesha utakatishaji wa fedha zinazotokana na biashara ya dawa za kulevya huwa na athari zaidi kwenye nchi masikini kuliko zile zilizoendelea. Utafiti uliofanywa na Shirika la Kimataifa linaloshughulikia Uchumi na Maendeleo "Organization for Economic Cooperation and Development" unaonesha ikiwa dola bilioni moja zitokananzo na biashara ya dawa za kulevya zitatakaswa (kuwekezwa kwenye shughuli halali) basi uchumi hushuka kwa kiasi cha asilimia 0.03 hadi 0.06.

**3. Rushwa**

Biashara ya dawa za kulevya imetawaliwa na rushwa katika kila ngazi. Kwa mfano, katika ngazi za uzalishaji, wakulima wa dawa za kulevya huweza kutoa

rushwa kwa wanaotakiwa kuharibu mashamba yao na iwapo watakamatwa watatoa rushwa kwa polisi au majaji. Vilevile, katika ngazi ya utengenezaji wa dawa za kulevya huweza kuwarubuni wafanyakazi wa viwanda vya kemikali kwa kuwapa rushwa ili waweze kupata kemikali bashirifu. Inapofikia ngazi ya usafirishaji wa dawa za kulevya, rushwa huweza kutolewa kwa wakaguzi wa mipakani kwa kutumia mianya iliyo katika sekta ya usafirishaji. Aidha, katika ngazi ya mtumaiji wa dawa za kulevya rushwa huweza kutolewa kwa madaktari na wafamasia hususani inapohusisha dawa za tiba zenye asili ya kulevya.

**4. Ugaidi na uasi**

Hali hii hutegemea na eneo ambalo kundi husika lipo. Makundi haya hunufaika zaidi iwapo yatakuwepo kwenye eneo lenye dawa za kulevya. Ili kuweza kumiliki eneo kubwa makundi haya huhitaji fedha nyingi na kujikuta wakitegemea mapato kutoka kwenye shughuli za kihalifu na biashara ya dawa za kulevya. Kwa mfano, kundi la ugaidi la Taliban linafadhiliwa na fedha itokanayo na kutoza kodi wakulima na wafanyabiashara wa afyuni (opium). Pia baadhi ya viongozi wa kundi hilo wametuhumiwa na Baraza la Umoja wa Mataifa kufanya biashara ya dawa za kulevya. Mwaka 2016, UNODC ilikadiria makundi ya uasi nchini Afghanstan kupata dola za kimarekani zipatazo milioni 150 kutokana na kodi walizowatoza wakulima na wafanyabiashara wa afyuni na heroin. Hatahivyo, inaaminika kuwa fedha ambayo makundi haya inapata kutokana na biashara ya dawa za kulevya kuwa ni kubwa zaidi. Kwa mfano, mwaka 2011, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilikadiria pato la Taliban kwa mwaka kuwafikia dola za kimarekani milioni 400, ambapo nusu yake ilisadikika kupatikana kutokana na kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya.

Kundi linguine la uasi lijulikananlo kama "The involvement of the Revolutionary Armed Forces of Colombia (FARC)" limekuwa likituhumiwa kupata fedha za kujiendesha kwa kujihusisha na biashara ya cocaine kwa miongo kadhaa. Kundi hili lilikuwa likilinda mashamba ya coca, kutoza kodi kemikali zinazotumika kutengenezea cocaine (kemikali bashirifu), kutoza ushuru ndege zinazotua kwenye viwanja vyake na kuuza cocaine.

Vyombo vya habari pia vimetoa ushahidi vikihusisha vikundi vya ugaidi na majeshi ya waasi na biashara ya dawa za kulevya. Mfano, makundi ya kigaidi ya IS na ISIS ya Iraq na Syria hutengeneza na kutumia dawa za kulevya ya "captagon" ya vidonge ambayo ni mchanganyiko wa amfetamini na caffeine. Boko haram nayo inatuhumiwa kuwasaidia wafanyabiashara wa heroin na cocaine kusafirisha dawa hizo katika eneo la Afrika Magharibi. Boko Haram walipohojiwa mahakamani nchini Chad ilielezwa kuwa walikutwa na dawa za kulevya na walikuwa wakiuza na kutumia dawa hizo. Katika eneo la

Kaskazini ya Afrika kundi la kigaidi la Al-Qaida lilihusishwa na biashara ya bangi na cocaine hususani kwa kuwalinda wasafirishaji ingawa mapato yaliyotokana na kujihusisha na dawa za kulevya hayakuwa makubwa sana. Kwa kawaida, makundi ya ugaidi na uasi huwa na vyanzo tofauti vya mapato. Iwapo fedha itokanayo na biashara ya dawa za kulevya itakosekana basi huweza kuteka watu ili walipwe fedha na kuwaachia, kuvamia benki, kuuza bidhaa za maliasili au rasilimali kale. Hatahivyo, makundi yanayovamia raia wasio na hatia hawahitaji kuwa na fedha nyingi ili kufanikisha azma yao.

# SURA YA TATU

## 3 TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA NA UDHIBITI WAKE NCHINI

### 3.1 UTANGULIZI

Tanzania inakabiliana na biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Dawa zinazozalishwa nchini ni bangi na mirungi na zinazoingizwa nchini ni heroin na cocaine. Dawa zinazoongoza kwa matumizi nchini ni bangi ikifuatiwa na heroin, mirungi na cocaine. Aidha, kumekuwa na wimbi la uingizwaji wa kemikali bashirifu nchini bila kufuata taratibu na hivyo kuleta shaka kwamba huenda zikawa zinatumika kutengeneza dawa za kulevya.

### 3.2 Tatizo la Biashara ya Dawa za Kulevya

Njia ya kusini ya kusafirisha heroin kutoka bara la Asia na kuingia Afrika Mashariki imeendelea kuwa chanzo kikuu cha uingizaji wa dawa za kulevya Afrika Mashariki hususan Tanzania. Dawa hizo za heroin ambazo zinapitishwa kwa njia hiyo hupelekwa nchi za bara la Asia, Ulaya na Amerika ya Kaskazini.

Katika kipindi cha mwaka 2017 Mamlaka imeimarisha udhibiti wa dawa za kulevya zinazopitia mipakani na kupunguza uingizaji wa dawa hizo nchini. Hali hii inadhihirishwa na ongezeko la dawa za kulevya zilizokamatwa ikiwemo heroin ambayo katika mwaka 2016 ilikamatwa kilo 42.26 ikilinganishwa na kilo 185.557 mwaka 2017 zilizokamatwa mwaka 2017 ikiwa ni mara nne zaidi.

#### 3.2.1 Ukamataji wa bangi na watuhumiwa


Takwimu zinaonesha kwamba kiasi cha bangi kilichokamatwa kimeshuka kutoka tani 68.23 kwa mwaka 2016 na kufikia tani 52.19 kwa mwaka 2017. Kushuka kwa kiasi kilichokamatwa kimechangiwa na juhudi zilizofanywa na vyombo vya dola katika kupambana biashara ya bangi. Vilevile, idadi ya watuhumiwa waliokamatwa wakijihusisha na bangi ilipungua kutoka 17,889 kwa mwaka 2016 hadi kufikia 11,528 kwa mwaka 2017.

Jedwali 2: Idadi ya Watuhumiwa na Kiasi cha Bangi kilichokamatwa 2007 - 2017

| Mwaka | Kiasi cha Bangi (Tani) | Idadi ya Watuhumiwa wa Bangi |
|---|---|---|
| 2007 | 60 | 7,161 |
| 2008 | 76.4 | 5,670 |
| 2009 | 56.2 | 3,382 |
| 2010 | 4.03 | 11 |
| 2011 | 17.3 | 39 |

| | | |
|---|---|---|
| 2012 | 48.7 | 5,548 |
| 2013 | 85.8 | 1,547 |
| 2014 | 81.3 | 11,918 |
| 2015 | 22.01 | 13,275 |
| 2016 | 68.23 | 17,889 |
| 2017 | 52.186 | 11,528 |

Grafu 1: Idadi ya Watuhumiwa na Kiasi cha Bangi kilichokamatwa 2007 - 2017





### 3.2.2 Ukamataji wa mirungi na watuhumiwa

Ukamataji wa mirungi uliongezeka kutoka tani 21.6 kwa mwaka 2016 hadi kufikia tani 67.8 kwa mwaka 2017 ikiwa ni ongezeko la zaidi ya mara tatu. Ongezeko hili lilichangiwa na operesheni nyingi zilizofanyika katika kupambana na biashara ya mirungi. Idadi ya watuhumiwa waliokamatwa wakijihusisha na mirungi ilipungua kutoka 2,397 kwa mwaka 2016 hadi kufikia 1,797 kwa mwaka 2017. Kupungua kwa watuhumiwa kunachangiwa na watuhumiwa wengi kukamatwa na kiasi kikubwa cha mirungi na baadhi ya mirungi kukamatwa bila wahusika kuwepo.

Jedwali 3: Idadi ya Watuhumiwa na Kiasi cha Mirungi kilichokamatwa 2007 - 2017

| Mwaka | Kiasi cha Mirungi (Tani) | Idadi ya Watuhumiwa wa Mirungi |
|---|---|---|
| 2007 | 2.2 | 648 |
| 2008 | 5.3 | 468 |
| 2009 | 22.9 | 365 |
| 2010 | 3.7 | 26 |
| 2011 | 0.1 | 100 |
| 2012 | 6.2 | 847 |
| 2013 | 12.8 | 581 |
| 2014 | 15.7 | 1,650 |
| 2015 | 16.6 | 1,780 |
| 2016 | 21.6 | 2,397 |
| 2017 | 67.8 | 1,797 |

Grafu 2: Idadi ya Watuhumiwa na Kiasi cha Mirungi kilichokamatwa Nchini 2007 - 2017




### 3.2.3 Ukamataji wa heroin na watuhumiwa


Jitihada kubwa za kupambana na biashara ya heroin ilifanikisha kuongezeka kwa ukamataji wa dawa hiyo kutoka kilo 42.26 mwaka 2016 na kufikia kilo 185.56 mwaka 2017 ikiwa ni kiasi kikubwa kuwahi kukamatwa kwa kipindi cha miaka

mitano iliyopita. Aidha, idadi ya watuhumiwa waliokamatwa wakijihusisha na heroin iliongezeka kutoka watu 716 kwa mwaka 2016 hadi kufikia watu 1,005 kwa mwaka 2017.

Jedwali 4: Idadi ya Watuhumiwa na Kiasi cha Heroin kilichokamatwa 2007 - 2017

| Mwaka | Kiasi cha Heroin (Kg) | Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin |
|---|---|---|
| 2007 | 16.2 | 254 |
| 2008 | 3.7 | 203 |
| 2009 | 9 | 122 |
| 2010 | 185.8 | 15 |
| 2011 | 264.26 | 20 |
| 2012 | 260 | 400 |
| 2013 | 36 | 75 |
| 2014 | 400 | 584 |
| 2015 | 64.75 | 474 |
| 2016 | 42.26 | 716 |
| 2017 | 185.557 | 1,005 |

Grafu 3: Idadi ya Watuhumiwa na Kiasi cha Heroin kilichokamatwa 2007 - 2017




### 3.2.4 Ukamataji wa cocaine na watuhumiwa


Kiasi cha cocaine kilichokamatwa kilipungua kutoka kilo 18.52 katika mwaka

2016 ikilinganishwa na kilo 4.143 zilizokamatwa mwaka 2017. Kuna uwezekano kuwa kiasi cha cocaine kilichokuwa kinaingizwa nchini kilipungua. Takwimu zinaonesha kuwa watuhumiwa wengi waliokamatwa wakijihusisha na cocaine kwa mwaka 2017 walikutwa na kiasi kidogo cha dawa hiyo.

Jedwali 5: Idadi ya Watuhumiwa na Kiasi cha Cocaine kilichokamatwa 2007 - 2017

| Mwaka | Kiasi cha Cocaine (Kg) | Idadi ya Watuhumiwa wa Cocaine |
|---|---|---|
| 2007 | 6.64 | 138 |
| 2008 | 3.5 | 251 |
| 2009 | 4.39 | 108 |
| 2010 | 62.97 | 8 |
| 2011 | 128 | 30 |
| 2012 | 151 | 138 |
| 2013 | 4 | 20 |
| 2014 | 45 | 351 |
| 2015 | 17.79 | 281 |
| 2016 | 18.52 | 263 |
| 2017 | 4.143 | 243 |

Grafu 4: Idadi ya Watuhumiwa na Kiasi cha Cocaine kilichokamatwa 2007 - 2017



Dawa nyingine za Kulevya zilizokamatwa ni gramu 6.5 za Mandrax zilizokamatwa jijini Dar es Salaam na kilo tano za bangi iliyosindikwa (hashish).

### 3.2.5 Uteketezaji wa mashamba ya bangi na mirungi

Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba, 2017 Mamlaka ikishirikiana na Jeshi la Polisi iliteketeza jumla ya mashamba ya bangi 230 yenye ukubwa wa ekari 646.5 ikilinganishwa na mashamba ya bangi 126 yenye ukubwa wa ekari 229.57 yaliyobainika mwaka 2016. Hilo ni ongezeko la mashamba 104 sawa na asilimia 82.5. Mikoa iliyoongoza kwa kilimo cha bangi ni Mara, Arusha, Njombe, Tanga, Simiyu, Rukwa, Geita na Morogoro. Katika kipindi hicho mashamba ya mirungi ya ukubwa wa ekari 64.5 yaliteketezwa huko Same mkoani Kilimanjaro.



***Picha ya 1:*** *Uteketezaji wa bangi iliyokamatwa.*

## 3.3 Udhibiti wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya

### 3.3.1 Kemikali bashirifu

Moja ya njia za kudhibiti uingizwaji holela wa kemikali bashirifu nchini ni kutoa vibali. Kwa mwaka 2017, makampuni 167 yalipewa vibali vya kuingiza kemikali bashirifu nchini. Aidha, kiasi cha tani 116,261.08 na lita za ujazo 13,016,466.7 za kemikali bashirifu ziliingizwa nchini kihalali kutoka katika nchi mbalimbali. Uingizwaji nchini kemikali hizi unahitaji udhibiti na usimamizi madhubuti ili kuhakikisha kwamba kemikali hizo zinatumika tu katika matumizi sahihi.

Katika kipindi hicho makampuni 77 yalifanyiwa ukaguzi katika mikoa kumi ya Tanzania bara. Mikoa hiyo ni Dodoma, Iringa, Arusha, Kilimanjaro, Dar es salaam, Tanga, Morogoro, Pwani, Mwanza na Mara ili kuhakiki mwenendo wa matumizi ya kemikali bashirifu na kutoa elimu juu ya madhara yanayoweza kusabishwa na matumiz mabaya ya kemikali hizo.

Katika ukaguzi huo jumla ya makampuni matatu yalipatikana na makosa mbalimbali ikiwemo kutokuwa na vibali vya kuingiza kemikali nchini. Aidha, asilimia 90 ya makampuni yote yalionekana kuwa na utunzaji mbaya wa kumbukumbu za kemikali. Jumla ya lita 304,513 na kilo 22,143 za kemikali bashirifu zilikamatwa.



***Picha ya 2:*** *Baadhi ya kemikali bashirifu zilizokamatwa zikiwa zimefunikwa na magunia ya pumba ikiwa ni mojawapo ya mbinu za wahalifu ili zisigundulike*

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na TFDA, na GCLA walibaini uchepushwaji wa kemikali bashirifu aina ya Pseudo-ephedrine kiasi cha kilo 8.358 katika kiwanda cha kutengeneza dawa za binadamu. Uchepushwaji huo ulisababisha kiwanda hicho kutengeneza dawa aina ya Coldril yenye kiwango kidogo cha kiambata hicho. Zaidi ya lita 10,000 za dawa hiyo zimezuiwa kwa uchunguzi zaidi.

#### 3.3.1.1 Mfumo wa udhibiti wa kemikali wa kielektroniki

Katika kipindi cha mwaka 2017, ulifanyika ufuatiliaji wa mienendo ya usafirishaji wa kemikali bashirifu kwa makampuni zaidi ya 40 kupitia mifumo ya kieletroniki na kubadilishana taarifa na taasisi za udhibiti za ndani na za kimataifa. Katika kipindi hicho, Mamlaka imeweza kufuatilia na kuchukua

hatua mbalimbali ikiwemo kuzuia uingizwaji nchini wa kemikali bashirifu zenye zaidi ya tani 500 kutoka nchi mbalimbali.

Aidha, marekebisho ya sheria yaliyofanyika mwaka 2017, yaliipa Mamlaka uwezo wa kufanya uchunguzi wa kimaabara ili kubaini dawa za kulevya na kemikali bashirifu zinazokamatwa, hatua ambayo itarahisisha na kuharakisha upelelezi wa kesi. Katika kutekeleza hili, Mamlaka ilianza mchakato wa kuanzisha maabara yake.

### 3.3.2 Udhibiti wa dawa tiba zenye asili ya kulevya

Dawa tiba zenye asili ya kulevya ni kama benzodiazepines (valiam), ketamine, tramadol na pethidine. Katika kudhibiti matumizi haramu ya dawa tiba zenye asili ya kulevya, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na Mamlaka ya Chakula na Dawa husimamia uingizwaji, usambazaji na matumizi ya dawa hizo. Udhibiti hufanyika kwa kufanya usajili, ukaguzi na utoaji wa vibali katika kampuni husika. Kwa mwaka 2017, jumla ya makampuni 222 yalikuwa yamesajiliwa kuingiza na kusambaza dawa tiba zenye asili ya kulevya nchini. Vilevile, makampuni 1,422 yalikuwa yamesajiliwa kusambaza dawa mbalimbali zikiwemo dawa tiba zenye asili ya kulevya.

Katika kipindi hicho ukaguzi ulifanyika katika kanda saba na kuweza kufikia vituo vya kutolea tiba 52 pamoja na viwanda viwili vya kutengeneza dawa za binadamu ili kufuatilia uhifadhi, matumizi na utunzaji sahihi wa kumbukumbu za matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya. Hatahivyo, katika ukaguzi uliofanyika kwenye mikoa ya Mwanza na Mara iligundulika uwepo wa uchepushaji wa dawa tiba aina ya Pethidine.

## 3.4 Tatizo la matumizi ya dawa za kulevya

Dawa za kulevya zinazotumika kwa wingi nchini ni bangi, heroin, mirungi, cocaine, viyeyushi (gundi na petroli) na dawa tiba zenye asili ya kulevya. Katika siku za karibuni kumeanza kujitokeza tatizo la kuongezeka kwa matumizi mabaya ya dawa tiba zenye asili ya kulevya kama vile benzodiazepines, ketamine tramadol na pethidine.

### 3.4.1 Takwimu za Watumiaji

Kutokana na makadirio yaliyofanyika mwaka 2014 kutokana na tafiti mbalimbali, Tanzania ilikadiriwa kuwa na watumiaji wa dawa za kulevya aina ya heroin kati ya 250,000 hadi 420,500 na kati yao 30,000 wakitumia dawa hiyo kwa kujidunga (Consesus Estimate on Key Population Size and HIV Prevalence in Tanzania). Wengi wa watumiaji wa heroin wanapatikana kwenye miji mikubwa hasa Dar es Salaam, Tanga, Mwanza, Mbeya, Pwani, Morogoro, Dodoma na Arusha.

### 3.4.2 Madhara ya dawa za kulevya

**Kiafya**

Utumiaji wa dawa za kulevya husababisha magonjwa ya akili, utegemezi (addiction), kinywa, moyo, ini, ngozi, mapafu na mengineyo. Kutokana na kuchangia vifaa vya kujidunga na kufanya ngono zisizo salama kwa ajili ya kujipatia pesa za kununulia dawa za kulevya huongeza kuenea kwa maambukizi ya VVU na virusi vya homa ya ini kwa watumiaji.

Vilevile kutokana na mazingira hatarishi ya matumizi ya dawa za kulevya, watumiaji wa dawa hizo wamekuwa na maambukizi ya kifua kikuu kulinganisha na jamii kwa ujumla. Matumizi ya kiwango kikubwa cha dawa za kulevya kuliko kilichozoeleka kwa mtumiaji, husababisha vifo vya ghafla hasa kwa wajidunga.

Watumiaji wa dawa za kulevya hasa wanawake wajawazito wamekuwa wakijifungua watoto wenye utegemezi wa dawa za kulevya na mara nyingi watoto wanaozaliwa wamekuwa na matatizo mengine ya kiafya yakiwemo ya akili na kuathiri ukuaji wao.

**Kijamii**

Dawa za kulevya zinasababisha mmomonyoko wa maadili katika jamii. Vijana ambao wanaishi kwenye jamii inayotumia na kufanya biashara ya dawa za kulevya wanaweza kujikuta wakitumia au kufanya biashara ya dawa hizi, hivyo kuharibika kwa kizazi kijacho. Matumizi ya dawa za kulevya yanachangia kuwepo kwa migogoro ya kifamilia katika jamii.

Watumiaji wamekuwa wakijihusisha na tabia na vitendo viovu vikiwemo wizi, uporaji, biashara ya ngono na ubakaji. Jamii imekuwa ikiamini kuwa matumizi ya dawa za kulevya ni jambo la kujitakia, hivyo kuwanyanyapaa na kuwabagua watumiaji jambo linalosababisha kuendeleza vitendo vyao vya uhalifu na utumiaji wa dawa za kulevya.

**Kiuchumi.**

Mfumuko wa bei ambao husababishwa na wenye fedha nyingi zinazotokana na dawa za kulevya kununua bidhaa kwa bei ya juu hivyo kufanya wananchi wenye kipato cha chini kushindwa kumudu gharama. Kuongezeka kwa tofauti kati ya wenye nacho na wasio nacho ambapo wenye fedha nyingi zinazotokana na biashara ya dawa za kulevya huweza kuhodhi sehemu kubwa ya rasilimali za jamii kama vile ardhi na kuwaacha wenye kipato cha kawaida bila chochote. Wenye kipato kikubwa kinachotokana na dawa za kulevya humudu kununua bidhaa nyingi kutoka nje ya nchi hivyo kufanya uchumi kudorora kutokana

na kutokuwepo na uwiano sahihi wa bidhaa zinazouzwa nchini na zile zinazoagizwa toka nje ya nchi. Ukwasi unaotokana na dawa za kulevya huchochea rushwa ambayo husababisha wafanyabiashara wa dawa za kulevya kuchukua fursa nyingi kama vile za kibiashara hivyo, huwaacha wawekezaji wenye kipato cha kawaida bila fursa. Vilevile, utakatishaji wa fedha zinazotokana na dawa za kulevya umekuwa chanzo kikubwa cha kuathiri uchumi wa nchi.

Matumizi ya dawa za kulevya huongeza mzigo kwa taifa kwa kuwa hupunguza nguvu kazi na husababisha uharibifu wa mali. Vilevile, gharama za udhibiti zikiwemo utoaji wa elimu kwa umma, uteketezaji wa mashamba ya bangi, uendeshaji wa kesi, kuwatunza wafungwa magerezani na kutibu uraibu na magonjwa yanayoambatana na utumiaji wa dawa za kulevya huongeza mzigo kwa taifa na jamii kwa ujumla. Aidha, husababisha utoro mashuleni au kazini, kusitisha masomo au kufukuzwa kazi na kuchangia kuongezeka kwa umaskini nchini.

Matumizi ya dawa za kulevya hudhoofisha afya za watumiaji ambao kundi kubwa ni vijana hivyo hushindwa kushiriki katika shughuli za uzalishaji kama vile kilimo na viwanda. Vilevile, matumizi ya dawa hizo huathiri sekta ya ajira kwa kuwa watumiaji walio kwenye ajira ufanisi wao hupungua hata wale ambao hawana ajira hawawezi kupata ajira kutokana na kuathiriwa na dawa za kulevya, hali hii hukwamisha ukuaji wa uchumi wa nchi.

**Kiusalama**

Watumiaji wa dawa za kulevya wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya kihalifu kama vile wizi, ukabaji na uporaji hivyo kusababisha maeneo yenye watumiaji wa dawa za kulevya kuwa na vurugu na kuyafanya si salama kwa kuishi. Matumizi ya dawa za kulevya kwa wanaoendesha vyombo vya usafiri wamekuwa wakisababisha ajali nyingi za barabarani na kupelekea uharibifu mkubwa wa mali na kugharimu maisha ya binadamu.

Fedha zinazopatikana kutokana na biashara ya dawa za kulevya hutumika kufadhili vikundi vya kigaidi; mfano kikundi cha kigaidi cha Taleban nchini Afghanistan hujihusisha na biashara ya heroin na fedha zinazopatikana hufadhili vitendo vya kigaidi sehemu mbali mbali duniani. Aidha, biashara ya dawa za kulevya huambatana na usafirishaji haramu wa binadamu ambapo wafanyabiashara wa dawa za kulevya wamekuwa wakifanya vitendo vya kikatili kwa kuwaweka rehani vijana wa kitanzania nje ya nchi ambao hupata mateso makali, ulemavu na wakati mwingine kuuawa pale biashara zisipofanikiwa.

**Kisiasa**
Wafanyabiashara wa dawa za kulevya baadhi yao wamekuwa wakijiingiza katika shughuli za kisiasa na hivyo kuwepo na uwezekano wa nchi kupata viongozi wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya. Pia, wafanyabiashara hao wanaweza kufadhili chaguzi na kuwaweka watu wao madarakani ili kulinda biashara zao. Hali hii huweza kuathiri mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

**Kidiplomasia**
Watanzania wapatao 1000 wamekamatwa katika nchi mbali mbali duniani wengi wao wakiwa China wakituhumiwa kujihusisha na dawa za kulevya katika nchi hizo. Hatua hiyo imechafua taswira ya nchi yetu katika medani za kimataifa. Watanzania wanapofika katika nchi za nje wamekuwa wakipata usumbufu mkubwa wa kupekuliwa zaidi kwa kudhaniwa kuwa wanaweza kuwa wamebeba dawa za kulevya.

**Kimazingira.**
Kilimo cha bangi na mirungi katika maeneo ya milima, misitu na kwenye vyanzo vya maji kimeendelea kuleta madhara makubwa ya kimazingira. Ukataji wa miti ya asili kwa ajili ya maandalizi ya mashamba ya bangi na mirungi hupunguza kiasi cha mvua, kuongeza joto na hatimaye kusababisha ukame. Madhara mengine yanayosababishwa na kilimo cha bangi na mirungi ni pamoja na kukauka kwa vyanzo vya maji, mmomonyoko wa ardhi na kutoweka kwa baadhi ya viumbe hai na uoto wa asili. Uharibifu huu umejidhihirisha katika baadhi ya safu za milima ya Uluguru, Usambara, Udzungwa na maeneo ya Arumeru.

Watumiaji wa dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga wamekuwa wakisababisha uchafuzi mkubwa wa mazingira katika maeneo wanayotumia kujidunga kama vile fukwe za bahari, vituo vya daladala, viwanja vya michezo na maeneo mengine mitaani, kwa kutupa ovyo mabomba ya sindano na kuongeza uwezekano wa kuambukizwa maradhi mbalimbali kwa jamii. Umwagaji ovyo wa kemikali zinazotumika kutengenezea dawa za kulevya huharibu mazingira, kuua viumbe hai na mimea pamoja na kuchafua maji ardhi.

### 3.4.3 Uelimishaji

**Mamlaka**
Mamlaka hutekeleza mkakati wa kuzuia watu wasijiingize katika matumizi ya dawa za kulevya kwa kutoa elimu kuhusu madhara ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya kwa makundi mbalimbali ya kijamii ikishirikiana na wadau. Elimu hii hutolewa kupitia vyombo vya habari, machapisho, maonesho ya kitaifa, semina na makongamano.

Elimu kwa umma ilitolewa kwenye maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani Juni, 2017 mkoani Dodoma; Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa maarufu kama Sabasaba, Wiki ya Vijana na Kilele cha Mbio za Mwenge Zanzibar, kongamano la vijana kitaifa lililoandaliwa na shirika la Save the Children jijini Dar es Salaam; Semina ya wanafunzi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Chuo Kikuu cha Dar es salaam (DUCE); Jubilei ya miaka 100 ya Uskauti Tanzania iliyofanyika mkoani Dodoma na Arusha pamoja na semina kwa wajumbe wa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA) jijini Dar es Salaam.

Semina elekezi ilitolewa kwa mawakili wa Serikali, waendesha mashtaka na wakuu wa upelelezi kuhusu ushughulikiaji wa kesi za dawa za kulevya na marekebisho yaliyofanywa kwenye Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, jijini Mwanza. Aidha, wadau kadhaa walijitokeza kuhaririwa maudhui ya vitabu na filamu vilivyokusudiwa kutumika kutoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya kwa walengwa mbalimbali.

**Elimu Iliyotolewa na Wadau**

Mashirika yasiyo ya kiserikali yamekuwa mstari wa mbele katika kushirikiana na Mamlaka katika kutoa elimu ya dawa za kulevya kwa njia za klabu za kupinga dawa za kulevya mashuleni, michezo, mikutano ya ustiri wa mihadarati, Unasihi, huduma za mikoba, kongamano na semina za uelimishaji rika kwa watumiaji wa dawa kulevya ili waweze kuachana kabisa na matumizi ya dawa za kulevya na kujijenga kiimani.

Mashirika ya Tanzania International Organization of Good Templars (T-IOGT) na Youth Achievement Village in Tanzania (YAVT) yalifungua klabu za kupinga dawa za kulevya katika shule mbalimbali za Dar es salaam. Wadau wengine waliotoa elimu ni; Kibwena Community Development (KICODE), Nurget Development Tanzania (NDT), Green kids and Youth Foundation, Peer to Peer Supporting Group (P2PSG), Alcoholic and Drug Addiction Organization (AADAO),

**Kimara Peer Educators and Health Promoters Trust Fund.**

Methadone Family Against Drug Abuse (MEFADA) iliwaandaa watumiaji wa dawa za kulevya ili waweze kupata tiba ya methadone, kutoa misaada ya kisheria na kufundisha afya ya uzazi. Tandika Youth Rehabilitation and Handcraft Group (TAYOHAG) ilifanya mikutano ya ustiri wa mihadarati ili kuwasaidia watumiaji na waliopata nafuu dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya. Asasi ya Elimisha Initiative ilitoa huduma ya kisaikolojia na unasihi katika nyumba tano za upataji nafuu (sober houses) na kutoa elimu kwa njia ya radio, televisheni na mitandao

ya kijamii. Youth Counseling and Rehabiliataion Centre (YCRC) ilitoa huduma kwa watoto na vijana walio katika mkinzano na sheria na wale walio katika hatari ya kukinzana na sheria.

## 3.5 Upunguzaji madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya (Harm reduction)

Moja ya mikakati mikuu ya kupambana na tatizo la dawa za kulevya nchini ni kupunguza madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya. Katika kutekeleza mkakati huo Mamlaka huratibu uandaaji wa miongozo mbalimbali, huduma za matibabu kwa waraibu na kutoa elimu ya kurekebisha tabia. Huduma zinazojihusisha na upunguzaji madhara nchini ni pamoja na tiba ya methadone, hatua 12 zinazotolewa kwenye nyumba za upataji nafuu na huduma za mikoba zikihusisha utoaji elimu juu ya tabia, ugawaji vifaa vya udungaji salama na utoaji rufaa kwa masuala ya kiafya, sheria, kisaikolojia, nk.

### 3.5.1 Tiba ya methadone

Kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na wadau wa maendeleo, Mamlaka imepunguza madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya kwa kupanua na kusimamia uendeshaji wa huduma ya methadone kwa waathirika wa dawa za kulevya nchini. Methadone ni tiba ya kisayansi kwa waathirika wa dawa ya kulevya aina ya heroin na imeidhinishwa na mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UNODC, WHO na UNAIDS. Tiba hii inasaidia katika kuondoa utegemezi wa dawa za kulevya. Huduma hii ilianza rasmi nchini mwaka 2011, hadi kufikia Desemba 2017, tiba ya Methadone imeweza kutolewa bure katika kliniki nne ambazo ni Muhimbili, Mwananyamala, Temeke na Mbeya. Jumla ya wategemezi wa dawa za kulevya 4,307 walipatiwa methadone na huduma za magonjwa yanayoambatana na matumizi ya dawa za kulevya katika kipindi hicho.

Mamlaka pia ilisimamia utafiti wa matumizi ya dawa ya methadone nyumbani badala ya kunywa dawa kituoni, ili kusaidia waathirika kupata huduma kwa urahisi zaidi. Aidha, Mamlaka imesimamia ununuzi, uagizaji, usambazaji, na utunzaji wa dawa ya methadone nchini kwa bei nafuu hivyo kupunguza gharama za manunuzi na uchepushaji wa dawa hiyo. Watumishi wa afya wapatao 150 walijengewa uwezo kwa kupewa mafunzo ya utoaji wa huduma ya methadone na kuboresha miundo mbinu katika hospitali ili kuanza kutoa huduma ya methadone.

Tiba ya Methadone inasaidia kupunguza utegemezi wa dawa ya kulevya aina ya heroin. Waathirika wanaopatiwa huduma hii pia hupewa huduma ya uchunguzi na matibabu ya magonjwa mengine kama vile; maambukizi ya VVU, homa ya

ini aina ya B na C, kutibu kifua kikuu, kifua kikuu sugu na magonjwa ya zinaa. Pia husaidia kupunguza uwezekano wa watumiaji kufa kwa kuzidisha kiwango cha dawa kutokana na matumizi ya dawa za kulevya. Waathirika wa dawa za kulevya hupata huduma nyingine za afya kama vile huduma za magonjwa ya akili, huduma za uzazi kwa mama na mtoto na huduma nyingine za kijamii. Tiba ya methadone imesaidia kupunguza mzunguko wa pesa chafu kwa wauzaji na wasambazaji wa dawa za Kulevya nchini na kuleta mabadiliko chanya ya kitabia na kupunguza vitendo vya kihalifu na uvunjifu wa amani kutokana na matumizi ya dawa za kulevya.

Kumekuwa na idadi kubwa ya wanaume kuliko wanawake wanaopata tiba ya methadone kwa sababu tatizo la matumizi ya dawa za kulevya huwakumba wanaume zaidi kuliko wanawake. Hali hiyo inadhihirika katika takwimu za waraibu waliopatiwa tiba ya methadone katika vituo husika. Majedwali yafuatayo yanaonesha mchanganuo wa waraibu waliofanikiwa kupata huduma ya tiba ya methadone katika vituo hivyo kwa mwaka 2017 pamoja jumla ya idadi ya waraibu ambao wamewahi kupatiwa tiba ya methadone tangu ilipoanzishwa katika vituo mbalimbali nchini.

**Jedwali 6: Waraibu Waliopata Huduma ya Methadone Tangu Kuanzishwa Hadi Mwaka 2017**

| Kituo | Waliosajiliwa | Wanaume | Wanawake |
|---|---|---|---|
| **Muhimbili** | 1,497 | 1,412 | 85 |
| **Mwananyamala** | 1,641 | 1,409 | 232 |
| **Temeke** | 1,139 | 1,078 | 61 |
| **Mbeya** | 30 | 26 | 04 |
| **Jumla kuu** | **4,307** | **3,925** | **382** |

**Jedwali 7: Waraibu Waliopata Huduma ya Methadone Nchini Januari - Desemba 2017**

| | Muhimbili | Mwananyamala | Temeke | Mwanza | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Waliosajiliwa** | 598 | 263 | 215 | 30 | **1,106** |
| **Wanaume** | 582 | 252 | 208 | 26 | **1,068** |
| **Wanawake** | 16 | 11 | 7 | 4 | **38** |

### 3.5.2 Nyumba za upataji nafuu (sober house)

Nyumba hizi zinaendeshwa na asasi zisizo za kiserikali ambapo waathirika wa aina mbalimbali za dawa za kulevya husaidiwa kuachana na matumizi ya dawa

hizo kwa kutumia hatua 12 za upataji nafuu bila kutumia dawa yoyote. Katika nyumba hizo waathirika hupatiwa unasihi, elimu ya dawa kulevya na stadi za maisha, na namna ya kuishi bila kutumia dawa za kulevya. Waathirika hulazimika kukaa katika nyumba hizo kwa kipindi kisichopungua miezi minne. Katika kipindi hicho pia hupatiwa mafunzo mbalimbali ya ujasiriamali. Mamlaka ina jukumu la kusimamia uanzishwaji na uendeshaji wa nyumba za upataji nafuu. Katika kipindi cha mwaka 2017 Mamlaka ilikamilisha mwongozo wa namna ya kuanzisha na kuendesha nyumba za upataji nafuu (The Guideline Manual of Standards for Establishing and Operating Sober Houses in Mainland Tanzania) ili nyumba hizo ziweze kuendeshwa kwa ufanisi zaidi. Hadi kufikia Desemba 2017 nyumba 24 zilianzishwa katika mikoa 11 ya Tanzania bara nyingi zikiwa katika jiji la Dar es Salaam.

Jedwali 8: Mikoa yenye Nyumba za Upataji Nafuu zinazotambuliwa na Mamlaka

| No. | Mkoa | Jina la Shirika | Jina la Nyumba |
|---|---|---|---|
| 1 | Arusha | Kipepeo Foundation | Treatment Centre S.H |
| | | Tz Sobriety and Chance Foundation | Arusha Recovery Community |
| | | | Meru Recovery Community |
| 2. | Dar es Salaam | Pillimisanah Foundation | Back to Life Sober House Na.1 |
| | | | Back to Life Sober House Na. 2 |
| | | | Back to Life Sober House Na. 3 |
| | | PEDDEREF | House of Wisdom |
| | | Drug Free Tanzania | Imani Sobriety Recovery Care Center |
| | | | Right Way |
| | | | The ties that bind us recovery centre |
| | | Kipepeo Foundation | South beach S. H |
| | | Tanzania Sobriety Initiative | |
| | | Morogoro Recovery Community TZ | MRC Na. 1 |
| | | | MRC Na. 2 |
| | | Changamoto ni Matumaini | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | New Vision of Life Society | |
| 3. | Dodoma | PEDDEREF | Dodoma S. H |
| 4. | Iringa | Iringa sober house | |
| 5. | Kagera | Sobriety Forever Reh. Center | |
| 6. | Kilimanjaro | Kipepeo Foundation | Treatment center S.H |
| | | Stay Clean Foundation | Good Will Recovery Community |
| | | | Northern Hill sober house |
| | | Kilimanjaro New Vision | |
| 7. | Morogoro | Kipepeo Foundation | Free at last S. H |
| 8. | Mwanza | Pillimisanah Foundation | Back to Life Sober House Na.4 |
| 9. | Pwani | Life and Hope Rehabilitation | |
| | | Filbert bay Foundation | |
| | | The Light of Miracle Organization | Women's of hope Rehabilitation |
| 10. | Tabora | Tabora Sober house | |
| 11. | Tanga | Tanga drug Free | Sober house Na. 1 |
| | | | Sober house Na. 2 |
| | | Gift of Hope Foundation | |

### 3.6 Masuala Mtambuka

Katika juhudi za kuimarisha udhibiti na usimamizi wa kemikali bashirifu nchini, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na taasisi nyingine imeanzisha mchakato wa kuhusisha sekta binafsi ili kufanya kazi pamoja na vyombo vya udhibiti wa kemikali hizo. Kwa mwaka 2017, Mamlaka kwa kushirikiana na vyombo vya udhibiti iliweza kupeleka baadhi watumishi kujifunza namna ya uanzishwaji wa ushirikiano na sekta binafsi kutoka katika nchi ambazo zinanufaika ambazo ni Ufaransa na Uswisi. Katika kuhakisha kwamba ushirikiano huo unaanzishwa nchini, Mamlaka za udhibiti ambazo ni DCEA, TFDA, GCLA, TRA, TPA, Jeshi la polisi

na Baraza la Wafamasia zimeungana pamoja kusimamia uanzishwaji wa ushirikiano huo.

Aidha, Mamlaka ilishiriki mikutano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa inayohusu udhibiti wa biashara na matumizi na tiba ya matumizi ya dawa za kulevya kwa kushirikiana na vyombo vya kimataifa kama vile INCB, UNODC na CND.

# SURA YA NNE

## 4 CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA BAADAYE

Udhibiti wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya kwa mwaka 2017 ulikuwa na mafanikio licha ya kuwepo kwa matatizo na changamoto mbalimbali. Sura hii imeainisha changamoto na mikakati iliyojiwekea Mamlaka katika kuongeza ufanisi wa udhibiti wa dawa za kulevya nchini.

### 4.1 Changamoto

1) Upungufu wa rasilimali watu na vitendea kazi,

2) Ukubwa wa mipaka na ukanda mrefu wa bahari ya Hindi unaosababisha udhibiti wa dawa za kulevya kuwa mgumu,

3) Kasi ya ukuaji wa teknolojia unaotumiwa na wauzaji na wasambazaji wa dawa za kulevya,

4) Uelewa mdogo na unyanyapaa juu ya tatizo la dawa za kulevya katika jamii,

5) Kukosekana kwa mfumo madhubuti wa ukusanyaji wa takwimu za ukubwa wa tatizo la dawa za kulevya, madhara na utoaji wa huduma za kijamii,

6) Ugumu wa tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya kutokana na uhusiano wa uraibu wa dawa za kulevya na maambukizi ya VVU, kifua kikuu, homa ya ini na magonjwa ya akili,

7) Ukosefu wa mfumo rasmi wa kuwajengea uwezo wa ujasiriamali wanaoacha matumizi ya dawa za kulevya baada ya tiba,

8) Kukinzana kwa sheria ya kudhibiti na kupambana dawa za kulevya katika nchi nyingine,

9) Upungufu wa vituo vya kutoa huduma za matibabu kwa watumiaji wa dawa za kulevya,

10) Upungufu wa rasilimali fedha hasa katika kusaidia asasi za kiraia zinazofanya kazi ya udhibiti wa dawa za kulevya.

## 4.2 Mikakati

1) Kuwajengea uwezo watendaji katika udhibiti wa dawa za kulevya ikiwemo kuwapatia mafunzo,

2) Kuinua uelewa kuhusu tatizo la dawa za kulevya na uchepushwaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya katika jamii kama vile kuanzisha klabu za mapambano dhidi ya dawa za kulevya mashuleni,

3) Kuhakikisha huduma za matibabu zinawafikia walengwa wengi zaidi,

4) Kuimarisha udhibiti wa dawa za kulevya kwa kutumia teknolojia ya kisasa ikiwemo kuanzisha maabara itakayotambua aina mbalimbali za dawa za kulevya pamoja na kubaini watumiaji wa dawa hizo,

5) Kuimarisha udhibiti wa matumizi na biashara ya dawa za kulevya ikiwemo kufanyia marekebisho Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na. 5 ya Mwaka 2015.

*Imeandaliwa na:-*

**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**
**8 Barabara ya Kivukoni, S.L.P. 80327, 11486 Dar es Salaam, Tanzania.**
**Simu+255 22 2152532, Fax:+255 22 2152820**
**Barua Pepe: cg@dcea.go.tz**